



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU - TAWALA ZA MIKOA NA
SERIKALI ZA MITAA

UCHAGUZI WA WANAFUNZI KIDATO CHA TANO 2014
AWAMU YA PILI

Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa imetangaza majina ya wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na kidato cha tano 2014 awamu ya pili.

Wanafunzi **8,101** wamechaguliwa kujiunga na kidato cha tano awamu ya pili 2014, kati ya hao **4,987** wamepangwa tahasusi za sayansi ya jamii na biashara na wanafunzi **3,114** wamepangwa tahasusi za sayansi.

Wanafunzi hawa wanatakiwa kuripoti kwenye shule walizopangiwa kuanzia tarehe **01 Septemba, 2014** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **15 Septemba, 2014**.

Imetolewa na Katibu Mkuu
OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI
29 AGOSTI, 2014